# Kielelezo cha taarifa kuhusu Watoto Wanaozaliwa kabla ya wakati Tanzania



## Nini maana ya kuzaliwa kabla ya muda (njiti)?

Kuzaliwa kabla ya muda ni pale mtoto anapozaliwa kabla ya kutimiza wiki 37 za ujauzito[1]. Nchini Tanzania, kifo kimoja kati ya vifo vinne vya watoto wachanga kinatokana na matatizo ya kuzaliwa njiti[4,a]. Kwa watoto njiti uwezekano wa kupoteza maisha katika wiki nne za mwanzo ni mara 6 hadi 26 ukilinganisha na wale wanaozaliwa baada ya kutimiza muda[3].

Zaidi ya hayo watoto njiti wanaoishi mara nyingi husumbuliwa na ulemavu wa kudumu kama vile uoni na usikivu hafifu, matatizo ya mapafu, matatizo ya moyo, matatizo katika kujifunza na tabia[1]. Kwa watoto, kuzaliwa kabla ya muda kuna matatizo makubwa sana katika makuzi na afya zao kama watoto na hata baadae wanapokua wakubwa.

### Tatizo la watoto njiti ni tatizo kubwa la kijamii Tanzania!

Tanzania inashika nafasi ya 12 kwa nchi zenye idadi kubwa ya watoto wanaozaliwa njiti ulimwenguni[4,]-kila mwaka watoto wachanga 213,500 huzaliwa kabla ya mimba kutimia wiki 37 tangu kutungwa[2,5,b] Ikiwa na maana ya kila watoto 9 wanaozaliwa hai, mmoja ni njiti.[2,5,b] Kuzaliwa njiti ni sababu ya pili kwa uzito inayochangia vifo vya watoto wachanga ndani ya mwezi wao wa kwanza wa uhai, kukiwa na vifo 9,400 vya watoto wachanga kwa sababu hiyo kila mwaka[2].

## Nini kinaweza kufanyika Tanzania?

Vifo vingi kati ya hivi vinaweza kuepukika kwa kuzuia watoto wasizaliwe kabla ya muda na uangalizi wa mtoto njiti:

- Kuzuia mimba za utotoni, mimba katika umri mkubwa, kuhakikisha muda wa kutosha kati ya mtoto na mwingine, kutibu magonjwa sugu na ya kuambukiza, kuepuka uzito hatarishi kabla ya ujauzito unaoongeza uwezekano wa kuzaa mtoto njiti.
- Mikakati ya uzazi wa mpango, ikiwemo nafasi ya kupumzika kati ya mtoto na mtoto na huduma rafiki kwa vijana kunaweza kupunguza uwezekano wa kuzaa mtoto njiti[1]. Kumnyonyesha mtoto kwa miezi 24 kunaweza kuzuia kubeba mimba baada ya muda mfupi na kuleta matokeo chanya kwa afya ya mama na mtoto mchanga[1].
- Huduma bora wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua, sambamba na huduma toka kwa wahudumu wenye ujuzi wakati wa kujifungua vinaweza kusaidia kupunguza vifo vitokanavyo na matatizo ya kujifungua mapema. Kuwekeza katika wahudumu wenye ujuzi na waliowezeshwa kwa vifaa ni muhimu pamoja na kuweka kipaumbele katika masaa 48 yanayozunguka kujifungua
- Kumsaidia mtoto mchanga kupumua, antibiotiki, huduma ya usafi wa kitovu, unyonyeshaji maziwa ya mama, huduma ya ngozi kwa ngozi kwa mama na mtoto, vyote ni vitu rahisi na vina uwezo mkubwa wa kuokoa watoto wagonjwa na wenye uzito mdogo[1].
- Kwa kutumia mbinu na teknolojia hizi ambazo kwa kiasi kikubwa ni rahisi na za ufanisi, zaidi ya robo tatu ya vifo vya watoto njiti vinaweza kuepukika sambamba na huduma bora kabla, wakati na baada ya kujifungua.

Mwaka 2014 Tanzania iliweka dhamira ya kutekeleza Mpango Kazi wa Kila Mtoto Mchanga[1] na Mpango Mkakati Ulioboreshwa[5].Mikakati hii inaonyesha wazi vipaumbele ambavyo ni suluhu kwa matatizo haya, inahimiza nguvu za pamoja ili kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo vya akinamama na watoto wachanga, na kuepusha tatizo la watoto wanazaliwa wafu. Ni wajibu wetu kuweka vipaumbele kulingana na ushahidi, vyenye gharama nafuu na vya kutekelezeka katika vituo vyote vya tiba vinavyohudumia wajawazito na kutoa huduma za kujifungua. Vile vile kuhakikisha ukusanyaji bora wa takwimu juu ya matokeo ya ujauzito ili kuwezesha hatua stahiki kuchukuliwa pale zinapohitajika zaidi.

**Kama mpango mkakati ulioboreshwa utatekelezwa, maisha ya watoto wachanga 9,400 yaweza kuokolewa na kuepusha watoto 2,500 kuzaliwa wafu na kuzuia vifo vya akina mama vipatavyo 1,400 ifikapo Desemba 2015**

## Watoto njiti Tanzania

| | |
|---|---|
| **Idadi ya vifo vya watoto wachanga ndani ya mwezi mmoja (2013)[6]** | **38,600** |
| Kiwango cha vifo ndani ya mwezi mmoja (2013)[2] | 21 kwa kila vizazi hai 1000 |
| **Kiwango cha kuzaliwa watoto kabla ya muda (njiti) (2010)4** | **11.4% ya watoto wanaozaliwa hai** |
| Nafasi ya nchi kwa kiwango cha kuzaliwa njiti (2010)[4] | 70 |
| **Idadi ya watoto wanaozaliwa kabla ya muda (2013)[2,5,b]** | **213,500** |
| Nafasi ya nchi katika dunia kwa kuzaa watoto kabla ya muda (2012)[2,5,b] | 12 |
| **Idadi ya vifo vitokanavyo na matatizo ya kuzaliwa kabla ya muda(2013)[4,c]** | **9,400** |
| Mchango wa vifo vya watoto vitokanavyo na kuzaliwa kabla ya muda katika vifo vya watoto wachanga(2013)[4,a] | 24% |
| **Mahitaji ya Uzazi wa Mpango yaliyokidhiwa[7]** | **58%** |
| Mahudhurio ya kliniki wakati wa ujauzito mara nne au zaidi (2010)[7] | 43% |
| **Kiwango cha kuhudumiwa na mhudumu mwenye ujuzi wakati wa kujifungua (2010)[7]** | **49%** |
| Kiwango cha akinamama na watoto wanaopata huduma ndani ya siku mbili baada ya uzazi (2010)[7] | 31% |
| **Kiwango cha kunyonyesha watoto wachanga maziwa ya mama mapema (ndani ya saa moja ya kuzaliwa)(2010)[7]** | **49%** |
| Kiwango cha kunyonyesha maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo (2010)[7] | 50% |

## Marejeo:


1. March of Dimes, The Partnership for Maternal Newborn & Child Health, Save the Children, World Health Organization. (2012). *Born Too Soon: The Global Action Report on Preterm Birth*. (Eds) Howson, C.P., Kinney, M.V., & Lawn, J.L. WHO: Geneva.
2. Blencowe, H., Cousens, S., Oestergaard, M. Z., Chou, D., Moller, A.-B., Narwal, R., Adler, A., Garcia, C.V., Rhode, S., Say,L., & Lawn, J. E. (2012). National, regional, and worldwide estimates of preterm birth rates in 2010 with time trends since 1990 for selected countries: a systematic analysis and implications. *The Lancet*, *379*(9832), 2162–2172.
3. Katz, J., Lee, A. C. C., Kozuki, N., Lawn, J. E., Cousens, S., Blencowe, H., Ezzati, M., Bhutta, Z., Marchant, T., Willey, B., Adair, L., Barros, F., Baqui, A., Christian, P., Fawzi, W., Gonzalez, R., Humphrey, J., Huybregts, L., Kolsteren, P., Mongkolchati, A., Mullany, L., Ndyomugyenyi, R., Nien, J., Osrin, D., Roberfroid, D., Sania, A., Schmiegelow, C., Silveira, M., Tielsch, J., Vaidya, A., Velaphi, S., Victora, C. G., Watson-Jones, D., & Black, R. E. (2013). Mortality risk in preterm and small-for-gestational-age infants in low-income and middle-income countries: a pooled country analysis. *The Lancet,* 382(9890), 417–25.
4. Liu, L., Oza, S., Hogan, D., Perin, J., Rudan, I., Lawn, J. E., Cousens, S., Mathers, C., & Black, R. E. (2014). Global, regional, and national causes of child mortality in 2000—13, with projections to inform post-2015 priorities: an updated systematic analysis. Supplementary appendix. *The Lancet, (Early online publication)*.
5. United Nations Population Division. (forthcoming, 2014). World Population Prospects: The 2013 Revision [estimates for 2013 used].
6. UNICEF. (2014). *Committing to Child Survival: Progress Report 2014 Committing to Child Survival: A Promise Renewed*. New York: United Nations Children's Fund.
7. National Bureau of Statistics [Tanzania], & ICF Macro. (2010). *Tanzania Demographic and Health Survey 2010*. Dar Es Salaam/Calverton: NBS, ICF Macro.
8. World Health Organization, & UNICEF. (2014). *Every Newborn: An Action Plan to End Preventable Deaths*. Geneva: WHO.
9. Ministry of Health and Social Welfare [United Republic of Tanzania]. (2014). *The National Road Map Strategic Plan to Accelerate Reduction of Maternal Newborn and Child Deaths in Tanzania 2008-2015. Sharpened One Plan April 2014*. Dar Es Salaam: MoHSW.


## Maelezo:

a. Inakadiriwa kuwa kulikuwa na vifo vya watoto wachanga 38,611 nchini Tanzania mwaka 2013 na idadi inayokadiriwa kwa vifo vitokanavyo na matatizo ya kuzaliwa kabla ya wakati ni 9,394. Makadirio haya ndiyo yametumiwa kukokotoa kiwango cha vifo vya watoto wachanga vitokanavyo na matatizo ya kuzaliwa kabla ya wakati: (9,394/38,611)*100=24% (takribani kifo kimoja kati ya vinne).

b. Pia inakadiriwa kuwa kulikuwa na vizazi hai 1,865,305 nchini Tanzania mwaka 2013 na kiwango cha kuzaliwa kabla ya wakati cha 11.4% mwaka 2010. Kama kiwango cha kuzaliwa kabla ya wakati cha mwaka 2010 kitatumiwa kwa idadi ya vizazi hai mwaka 2013: (11.4/100)*1,865,300=213,490 (inayokadiriwa kama 213,500). Kiwango cha kuzaliwa kabla ya wakati cha 11.4% ni sawa na mtoto mmoja njiti kwa kila vizazi hai 9. Nchi zinapangwa kutokana na idadi ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati kwa kutumia makadirio haya ya mwaka 2013.

c. Haya ni makadirio ya idadi ya vifo kutokana na matatizo ya kuzaliwa kabla ya wakati katika kipindi cha siku 28 za uhai nchini Tanzania (iliyokadiriwa kutoka 9,394).[4] Kama idadi ya vifo kutokana na matatizo ya kuzaliwa kabla ya wakati kutahusisha watoto toka kuzaliwa hadi miaka mitano, idadi hii inakuwa 10,800 (Makadirio ya Save the Children).

**Novemba 2014**